# NOA BONGO, JENGA MAISHA YAKO
# "KABUMBU AFRIKA - NI ZAIDI YA MCHEZO!"

## KIPINDI CHA KUMI: "Vipanga na Vifaranga"

**MWANDISHI: Chrispin Mwakideu**

**WAHARIRI: Andrea Schmidt, Maja Braun**

**Orodha ya wahusika/ KIPINDI CHA KUMI**

- Msimulizi

**SCENE ONE: CHANGING ROOMS AT CITY STADIUM**
- Chedede (mume,14)
- Safina (mke,13)
- Jonathan (mume,15)
- Metogba (mume, 28)
- Ajenti/ dalali (mwenye lafudhi ya kiropa. mume, 40+)

**SCENE TWO: ON THE STREETS OF TAMBARARE CITY**
- Mr.Wakasa (mwenyekiti uongozi wa soka. mume, 54)
- Mtangazaji spoti (mke, 25)

**SCENE THREE: BACK IN THE CHANGING ROOMS**
- Jonathan (mume,15)
- Metogba (mume, 28)

**SCENE FOUR: AT AUNT LILY'S**
- Mhe. Makemba. (mume,55)
- Shangazi Lily (mke, 33)

**SCENE FIVE: AT THE AIRPORT**
- Chedede (mume,14)
- Safina (mke,13)
- Jonathan (mume,15)
- Mhe. Makemba. (mume,55)
- Shangazi Lily (mke, 33)

**INTRO:**

1. **MSIMULIZI:** Salaam tele na karibuni katika Noa bongo, jenga maisha yako. Hiki ni kipindi cha kumi na cha mwisho katika makala ya, **"Kabumbu Afrika - Ni zaidi ya mchezo!"** Katika kipindi kilichopita mchuano kati ya wachezaji chipukizi wa kliniki ya soka na mabingwa Tambarare F.C. ulisimamishwa baada ya wahalifu kuuvamia uwanja wa michezo baada ya Chedede kuifungia bao timu yake. Uhusiano wa Mh. Makemba na mwanawe wa kiume Jonathan umezidi kuvurugika kwasababu ya mkono wake katika kukamatwa Chedede. Kwa upande mwengine, Komora asema ukweli wake baada ya Chedede aliyekuwa rafikiyake mkubwa kumtembelea katika kituo cha polisi. Na shangazi Lily bado anakataa kumfafanulia Mhe. Makemba tukio fulani la awali. Jee itakuaje? Baki nasi tunapoianza makala hii katika vyumba via kugeuzia sare.

**SCENE ONE: CHANGING ROOMS AT THE CITY STADIUM**

**2. SFX: MURMURS AND VOICES FROM THE YOUNG PLAYERS**

**3. METOGBA:** Poleni kwa yaliotokea uwanjani. Sio makosa yenu. Muliwafunga mabingwa na baadhi ya wahalifu hawakulikubali hilo.Mumenipa fahari sana. Fursa Sasa ni ya kumteua mchezaji stadi kabisa kati yenu.

4. **MSIMULIZI**: Wakati Metogba akijiandaa kumtaja mchezaji bora katika kiliniki ya soka, Mhe. Makemba alifanikiwa kufika alipokuwa shangazi Lily na, akisaidiwa na walinzi wake akawahi kumtoa na kumuingiza garini mwake. Kwanza lakini, katika chumba cha kugeuzia sare...

5. **METOGBA:** Nyote mutakubaliana nami kuwa mchezaji bora ...

6. **SFX: DOOR BEING OPENED**

7. **AJENTI: (European accent)** Nawasalimu nyote! Mimi ni wakala wa soka na nimefurahishwa sana na uchezaji wenu. Kwa bahati mbaya mechi ilikuwa fupi. Sitachukuwa muda wenu mrefu. Nafikiri nyote munajuwa lengo langu kuwa hapa. Hii hapa ni...

8. **SFX: FOLDER/FILE BEING OPENED, PAPERS SHUFFLING**

9. **AJENTI:** Huu hapa ni mkataba wa yule kijana aliyefunga bao la pekee katika mechi hiyo. Unaweza kutia saini sasa. Baada ya hapa nitaanza maandalizi ya safari yako na kucheza barani Ulaya.

10. **METOGBA:** Uhm... bwana, kidogo umechelewa. Mchezaji unayetaka kumsajili ndiye huyohuyo ninayetaka kumtangaza kama mchezaji stadi, naye ni Chedede. Sasa Dede, ukipenda unaweza kujiunga na timu ya chipukizi mpaka utakapotimia umri wa miaka 18.

11. **SFX: HUGE APPALAUSE FOLLOWED BY CHANTS OF 'DEDE"**

**12. SAFINA:** Hongera sana Dede! Umefanikiwa! Kweli umefanikiwa!

**13. AJENTI:** Sawa, kwa nini tusimuache aamue mwenyewe basi? Chedede una mawazo gani? Utauchukua mkataba wangu au utajiunga na timu ya wachezaji chipukizi? Hii inaweza kuwa nafasi yako muhimu!

**14. CHEDEDE: (Confused)** Sijui. Yote yanatokea kwa kasi sana, nipeni muda.

**15. AJENTI:** Kwa bahati mbaya sina muda. Nasafiri leo usiku na ni lazima mkataba uwe umetiwa saini nirudi nao. Sasa ikiwa hutaweza naweza kumpa nafasi yule mchezaji aliyepiga ile kona? Samahani... Silijui jina... Wewe! Ndio, wewe hapo!

**16. JONATHAN: (Shocked)** Mimi? Jonathan. Jina langu ni Jonathan. **(Very excited)** Ndio! Ningependa kutia saini mkataba… niko tayari.

**17. AJENTI:** Vyema! Sasa, makaratasi ndio haya. Huna haja ya kusoma chochote. Kila kitu kimeshughulikiwa. Tia saini hapo mwisho palipoandikwa "mchezaji".

**18. SFX: PAPERS BEING FLIPPED OVER PAGE BY PAGE**

**19. METOGBA:** Kama haitakuwa tatizo naomba nizungumze na wachezaji wangu kwanza kwa faragha.

**20. AJENTI:** Tayari nimemaliza. Nitachukua makaratasi baada ya Jonathan kuyatia saini kisha nitaondoka.

21. **METOGBA:** Sawa, nakuelewa.Lakini naomba utupe dakika moja tu, kabla Jonathan hajatia saini popote.

22. **AJENTI:** Haya basi. Nasubiri hapo nje.

23. **MSIMULIZI**: Wachezaji wengi huangukia mikononi mwa mawakala tapeli wanaowapa mikataba bandia inayowaahidi makuu badala yake inakuwa dhiki tupu. Jee huu ni kama hiyo? Jee vipi jinsi ya kuiepuka? Jibu tutalipata baada ya muda usio mrefu. Kwanza, tujiunge na Mhe. Makemba na shangazi Lily wakiwa ndani ya gari wanasikiza habari moto moto zilizowafikia muda huo...

## SCENE TWO: ON THE STREETS OF TAMBARARE CITY

**24. SFX: CAR DRIVING SOUND FROM INSIDE. FADES IN BACKGROUND AS PRESENTER TALKS**

**25. SPORTS NEWS PRESENTER:** Karibu tena, mpenzi msikilizaji, katika kituo chako cha kitaifa. Kama tulivyowaeleza, mchuano baina ya timu ya Tambarare F.C. na timu ya muda ya wachezaji chipukizi wa kiliniki ya soka, ulisimamishwa baada ya mashabiki wa Tambarare F.C. kusababisha vurugu baada ya timu yao kufungwa bao moja. Mechi hiyo ilihudhuriwa pia na Raisi wa nchi yetu. Pamoja nami hapa kulizungumzia suala hili ni Bwana Wakasa, mwenyekiti wa Shirikisho la Soka nchini. Karibu Bwana Wakasa.

**26. WAKASA:** Asante.

**27. MTANGAZAJI SPOTI:** Sasa, mutachukua hatua gani kuwaadhibu waliosababisha kitendo hiki cha kinyama na kiholela?

**28. WAKASA:** Kwanza kabisa tumebahatika kuwa hakuna aliyejeruhiwa katika vurugu hizo. Pili, kama mwenyekiti wa shirika linalosimamia soka nchini navilaani kabisa vitendo hivyo vya wahalifu na shirikisho litafanya kikao

katika siku zijazo nipo liweze kuwaadhibu vikali wataopatikana na hatia.

**29. MTANGAZAJI SPOTI:**Jee hii ina maana kuwa timu ya Tambarare F.C. pia itaadhibiwa?

**30. WAKASA:** Sitayazungumzia hayo kwa sasa. Nataka kuwahakikishia mashabiki wa soka kuwa uchunguzi kamili utafanyika na watakaotiwa lawamani watachukuliwa hatua za kisheria pasina kuzingatia cheo, umaarufu wala utajiri.

**31. MTANGAZAJI SPOTI:** Tunaweza kuzungumzia kuhusu huyu mchezaji chipukizi aliyefunga bao... (**Discussion fades out)**

**32. SFX: CAR DRIVING**

**33. MSIMULIZI:** Wakati mahojiano yakiendelea hewani, katika chumba cha kugeuzia sare...

**<u>SCENE THREE: BACK IN THE CHANGING ROOMS</u>**

**34. METOGBA:** Jonathan una wazimu? Vipi utautia saini mkataba ambao hujausoma? Nisikizeni nyote. Najua nyote muna ndoto za kuwa wachezaji bora Afrika. Lakini jihadharini …mambo si kama munavyoyadhania huko Ulaya.

**35. JONATHAN:** Lakini... lakini, mkufunzi... huyu wakala ametoka Ulaya, sidhani kuna matatizo. Huko ndio wachezaji wazuri wanakokimbilia.

**36. METOGBA:** Kwa hivyo? Yaani kwa kuwa ametoka Ulaya ndio munamuamini bila sababu? Wacha niwaambie ukweli. Sio nyote mutafanikiwa kuwa wachezaji maarufu wa kulipwa. Lakini musimpe mtu yeyote nafasi ya kuwadhulumu. Jonathan sitakulazimisha, ila chukua muda, usome mkataba kwa makini na ukikubaliana na masharti yake ndipo uutie saini... ushauri huo ni kwako wewe pia… Chedede.

**37. MSIMULIZI**: Metogba amesema kweli. Yote yanayomeremeta si dhahabu. Na kabla ya kutia saini, soma na uelewe. Kama hujaelewa chochote, muuulize yeyote Alice na ufahamu akufafanulie. Jonathan aliutilia maanani ushauri Metogba na akaghairi kuutia saini mkataba huo. Baadaye kidogo, gari ya Mhe. Makemba iliwasili nje ya nyumba ya shangazi Lily.

**SCENE FOUR: AT AUNT LILY’S**

**38. SFX: CAR COMES TO A HALT… DOOR OPENS.**

**39. SHANGAZI LILY:** Asante kwa kunileta, na kuninusuru pale uwanjani...

40. **MHE. MAKEMBA:** Karibu. Sasa, hutaki kunieleza chochote kuhusu mimba yako uliyokuwa nayo? Uliiavya au vipi? Nimeshaomba msamaha kwa kukuwacha peke yako nataka tu ukweli na nitakuacha kwa amani.

41. **SHANGAZI LILY:** Kwani kipofu? Sawa. Nitakueleza. Sikuavya mimba. Nilizaa mtoto wa kiume, nikampa jina na nikatoroka; kama babake. **(Sadly)** Uamuzi huo ulikuwa mbaya sana kwa maisha yangu.

**42.** **MHE. MAKEMBA:** **(Excited)** Anaitwaje? nitamtafuta. Ulimpa jina lipi?

**43.** **SHANGAZI LILY:** Hakuna haja ya kumtafuta, unamjua vizuri sana. Ulimuona leo akifunga bao muhimu.

**44. SFX: CAR DOOR SHUT**

45. **MSIMULIZI:** Mshtuko, hatia, na kuchanganyikiwa. Mhe. Makemba alivihisi vyote hivyo. Maisha yake ya awali yalimjia tena baada ya kutoweka kwa muda ulioonekana kuwa mrefu. Baada ya majuma machache, siku ilifika ya wachezaji chipukizi kuelekea Ulaya. Wote walikusanyika kwenye uwanja wa ndege wakiwa na wingi wa bashasha, wamezungukwa na waandishi wa habari, familia, marafiki na mashabiki wa soka.....

## SCENE FIVE:AT THE AIRPORT

46. **SFX: AIRPORT SOUNDS, ANNOUNCEMENTS IN THE BACKGROUND**

47. **JONATHAN:** Nina bahati, sikuutia saini ule mkataba. Ningekuwa ninafanya kazi katika mkahawa siku tano na kucheza mpira kwa siku mbili pekee kwa wiki! Na yote hayo bila malipo!

**48.** **CHEDEDE:** Naam, lakini usiwe na shaka. Nina hakika utapata timu nyengine tukifika Ulaya. Aah Safina yule yuaja na shangazi yake...

**49.** **SAFINA:** Habari, mchezaji maarufu. **(Cheerfully)** Jonathan hujambo? Habari nyote!

**50.** **JONATHAN:** Salama, jamani, tuingieni sasa. Kwa heri baba!

**51.** **MHE. MAKEMBA:** Kwaheri kijana wangu. Safari njema na kila la heri.

**52.** **SAFINA:** Kwa heri shangazi Lily, nisalimie mama nyumbani.

**53.** **SHANGAZI LILY:** Kwa heri Safina. Jitunze huko uendako.

**54.** **CHEDEDE:** **(Sadly)** Uhm... kwa herini.

**55. SHANGAZI LILY / MHE. MAKEMBA: (Whisper)** Kwa heri kijana wetu!

**<u>OUTRO</u>:**

**56. MSIMULIZI:** Baadaye, ndege ilipopaa kutokea uwanja wa ndege wa Tambarare , Chedede alitiririkwa na machozi alipoyakumbuka hayo maneno yaliyotamkwa na Shangazi Lily pamoja na Mhe. Makemba. Kisha ghafla swali likamjia, je Mheshima Makemba na shangazi Lily walikuwa wazazi wake wa kweli?au wanataka kunufaika na mafanikio yake mapya? Lakini hiyo ni hadithi ya siku nyengine, kwa sasa tumefikia hatima ya kipindi cha **"Kabumbu Afrika! Ni zaidi ya mchezo!".** Mwandishi wa kipindi hiki cha redio ni Chrispin Mwakideu. Natumai umeyafurahia makala na tunakualika kutupa maoni, mawazo na hata matukio ya binafsi kuyahusu au kandanda kwa jumla nchini mwako, kupitia kurasa za tovuti zetu www.dw-world.de/lbe. Shukran na endelea kushangilia kabumbu yetu!